



The Land Charter



THE CHARTER FOR SECURE AND EQUITABLE ACCESS TO LAND AND NATURAL RESOURCES IN KENYA

'For sustainable development in Kenya, the people of Kenya demand that Political Parties vying in the 2007 General Elections commit through their manifestos to protect and promote secure and equitable land rights'

RECOGNIZING that LAND:

- is the basis of livelihoods security for vast majority of Kenyans who depend on it as farmers, pastoralists, fisher-folk and forest-dwelling hunter-gatherers
- is the foundation of our national economic development through agriculture and pastoralism, tourism, mining, fisheries and the exploitation of other natural resources
- defines our history as well as the cultural, social, economic and political relations within our society
- is potentially a major source of conflict due to increased pressure arising from high population growth, competing land uses, climate change and environmental and natural resources degradation
- reforms and a supportive National Land Policy have a critical bearing on our capacity to manage the land related challenges for economic development and poverty reduction in both rural and urban areas of Kenya.

We,
a political party vying for leadership of Kenya in the 2007 General Elections promise to incorporate the Land Charter into our Party Election Manifesto and to dedicate our energy to the adoption and implementation of a National Land Policy to secure land rights in order to promote secure livelihoods, increased investment in the land sector and sustainable development.

Further, we promise the people of Kenya THAT:

1. We shall promote a model of rural development based on enhancement of the productive capacities of rural population and the strengthening of local economies. Economic efficiency shall be supportive of social efficiency and markets, including land markets that enhance local productive relations and do not lead to inequitable concentration of wealth. In this connection we commit to securing the land and resource rights of the rural poor as a necessary condition for economic growth.
2. We shall allocate and/or advocate for allocation of sufficient resources for effective implementation of the National Land Policy once adopted,

including the recognition of community land tenure and putting in place the legal and institutional framework for its operationalization.

3. Equity shall be a fundamental goal of all land policies supported by our party. Policies encapsulated in the National Land Policy shall and must promote gender, generational and ethnic equity as a basis for people-centered sustainable development. In particular our party shall ensure law, policy and practice secure the rights of women, who are the main users of land in most parts of the country. Historical injustices shall be addressed and land redistribution programmes designed and implemented where needed.
4. Processes of land institutional transformation shall be accompanied by democratization of institutions that govern land and resources, at all levels of government and society. This will entail both devolution of decision-making authority, and lobbying for allocation of adequate resources to decentralized institutions.
5. We shall strive for the accountability of all development actors, including developed countries and International Financial Institutions towards the realization of meaningful land and resource rights. In this connection we shall take concrete steps to build the capacity of Kenya to address the challenges of globalization with due regard to social equity for the poor. We shall also campaign for an end to the wealthy nations' demand to liberalize agricultural markets, while they continue to subsidise their farmers as a means of protecting them from competition.
6. We shall recognize and support the right of marginalized and vulnerable groups to organize themselves against the negative effects of inappropriate policies, and to campaign for appropriate alternatives. We commit to working closely with such groups and to ensuring they receive appropriate assistance and support.
7. We shall domesticate and/or advocate for domestication of International Agreements but with due regard to the interests of communities that depend on land and natural resources for their livelihoods. We shall mobilize a common national voice against the International Agreements that endanger these rights and interests as well as ensure that our engagement with the International Policies and agencies are aimed primarily at enhancing rights of our local communities.

- 8. We acknowledge that land and natural resource issues are multi-dimensional and cannot be reduced to a single disciplinary or sector-specific approach. We shall promote the building of strong and equitable partnerships of researchers and practitioners in the public sector, private sector, CSOs and academic institutions.
- 9. We commit to fast-track the above land reforms within the first two years of our term in office

'No sustainable development without real rights in a National Land Policy'

Name of Party Leader

Signature.....

Date.....

Official Party Seal/Stamp

Witnessed by KLA National Co-ordinator.....

On behalf of Kenya Land Alliance and its membership

Signature.....

Date.....

Official Rubber Stamp

This charter is KLA civic engagement tool with Political Parties vying in the 2007 General Elections in firm belief that its incorporation and adoption by Political Leaders shall contribute to greater political commitment to land reforms essential to productivity, greater food security, higher income, more sustainable land use and a more vibrant economy in Kenya.

MKATABA WA KIUSALAMA NA USAWA WA KUPATA ARDHI NA MALIASILI NCHINI KENYA

'Ili kuwa na maendeleo endelevu humu nchini, wakenya wanavitaka vyama vya kisiasa vitakavyojihusisha na Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka wa 2007, watoe hakikisho kupitia kwa manifesto zao kwamba watalinda na kuendeleza usalama na usawa wa haki za ardhi'

KWA KUTAMBUA yakwamba ARDHI:

- Ndio msingi wa usalama wa maisha ya Wakenya wengi wanaoitategemea ardhi kama vile wakulima, jamii ya wafugaji, wavuvi na hata wakaaji wa maeneo ya misitu ambao pia ni wasasi.
- Ndio msingi wa uchumi na maendeleo ya kitaifa kupitia kwenye kilimo na ufugaji, utalii, uchimbaji madini, uvuvi na utafutaji wa maliasili nyinginezo.
- Inaifafanua kwa kina historia yetu na hali kadhalika tamaduni, ujamaa, uchumi na uhusiano wa kisiasa katika jamii yetu.
- Ina uwezo wa kuzua mifarakano na fujo kutokana na msukumo wa ongezeko la idadi ya watu, mashindano yanayoibuka kutokana na matumizi ya ardhi, mabadiliko ya kimsimu na kudhoofika kwa mazingira na maliasili
- Kuwepo kwa mabadiliko na Sera ya Kitaifa ya Ardhi iliyo madhubuti, kutaleta mageuzi yanayofaa katika kusimamia na kuzithibiti changamoto za masuala ya ardhi, kwa minajili ya maendeleo ya kiuchumi na kuangamiza umaskini katika maeneo ya miji na mashambani humu nchini

Sisi,
Chama cha kisiasa kinachopigania uongozi wa taifa la Kenya katika **Uchaguzi Mkuu wa 2007**, tunaahidi kuhusisha Mkataba wa Ardhi kwenye Manifesto ya Uchaguzi wa Chama na kujitolea kwa moyo mmoja katika kuhusisha na kuwajibisha **Sera ya Kitaifa ya Ardhi** ili kuupata usalama wa haki za ardhi na kuimarisha maisha ya kijamii, kuboresha uwekezaji katika sekta ya ardhi na kuimarisha maendeleo endelevu.

Licha ya hayo, tunaahidi wananchi wa Kenya YAKWAMBA:

1. Tutaendeleza mfumo wa maendeleo ya mashinani kulingana na kiwango cha uzalishaji kwenye maeneo yote na kuboresha uchumi wilayani. Ubora wa kiuchumi utasaidia ubora wa kijamii na masoko yaliyopo, ikiwa ni pamoja na masoko ya ardhi yatakayoimarisha uhusiano bora utendakazi wilayani na ambayo haitapelekea kutokuwepo kwa usawa wa kiutajiri. Kwa misingi hii, tunatoa hakikisho kwamba tutalinda haki za ardhi na maliasili ya mwananchi maskini mashinani kama chombo muhimu cha maendeleo ya kiuchumi.

2. Tutatenga na pia kupigia debe kutengewa rasilimali ya kutosha itakayosaidia kuhusisha Sera ya Kitaifa ya Ardhi pindi tu itakapoambatanishwa, ikiwa ni pamoja na kufahamika kwa kipindi cha umiliki wa ardhi za kijamii na kuwepo kwa mifumo mahususi ya kisheria na kiasasi ili kuiwezesha kutekelezeka.
3. Usawa utakuwa ndio lengo la kimsingi na sera zote za ardhi zitaungwa mkono na chama chetu. Sera zilizoambatanishwa katika Sera ya Kitaifa ya Ardhi, lazima zipigie upatu masuala ya kijinsia, usasa na usawa wa kiukabila, kama kigezo muhimu cha maendeleo endelevi ya maelewano kwa wananchi. Kwa hakika, chama chetu kitahakikisha kwamba sheria, sera, na kuendeleza haki za usalama wa wanawake, ambao ndio watumiaji wakuu wa ardhi katika maeneo mengi ya nchi. Unyanyasaji wa kihistoria utazungumziwa na mipango ya ugawanyaji wa ardhi itapangwa na kutekelezwa ipasavyo.
4. Taratibu za kiasasi za mabadiliko ya ardhi zitahusishwa kwa kuingiza demokrasia kwenye asasi hizo ambazo zitalinda ardhi na rasilimali zake, katika ngazi zote za kiserikali na kijamii. Suala hili litahusisha kuwepo halmashauri ya ugawanyaji na utoaji-maamuzi, na kupigia upatu mgao wa kutosha wa rasilimali kupelekewa asasi zilizopewa mamlaka.
5. Tutajitahidi ili tujiwajibishe na wahusika wengine wa kimaendeleo, ikiwa ni pamoja na Mataifa Yaliyoendelea na Asasi za Kifedha za Kimataifa katika kufahamu umuhimu wa haki za ardhi na rasilimali zake. Katika misingi hii, tutachukua hatua kabambe ili kujenga uwezo wa taifa la Kenya kuweza kujikwamua kutokamana na changamoto za kiutandawazi, huku tukitegemea usawa wa Kijamii kwa walio maskini. Kadhalika tutafanya kampeini ya kukomesha “mataifa ya mabwenyenye” kupigania usawa wa masoko ya kilimo huku wakiwapunguzia na kulinda maslahi ya wakulima wao kutokana na mashindano ya kibiashara.
6. Tutakubali na kupigania haki za maskini na watu waliotengwa kwenye jamii ili kuwawezesha kukabiliana na sera zisizo na usawa, na kufanya kampeini kwa sera m’badala. Tunaahidi kufanya kazi kwa kushirikiana na wananchi hao ili kuhakikisha kwamba wanapata msaada na usaidizi unaofaa.
7. Tutaonyesha na pia kupigia upatu uyeyushaji wa mikataba ya kimataifa, huku yakizingatiwa mahitaji ya jamii mbali mbali inayotegemea ardhi na maliasili yake kwa maisha yao ya kila siku. Tutajitahidi kuwa na sauti moja dhidi ya mikataba hiyo ya kimataifa ambayo inaathiri haki hizi na mahitaji na hali kadhalika hakikisha ya kuwa uhusiano wetu na sera za kimataifa na mawakala zitalenga kuboresha haki kwa jamii yetu.

8. Tunafahamu kuwa masuala ya ardhi na maliasili yana mielekeo tofauti tofauti na hayawezi kufanywa kuwa masuala ya mfumo au muelekeo mmoja. Tutajishughulisha na ujenzi madhubuti na ushirika wenye usawa kwa watafiti na waendesha biashara katika sekta ya umma, sekta ya kibinafsi, mashirika ya kijamii na asasi za kielimu.
9. Tunaahidi kutekeleza na kupigania mabadiliko ya sera ya ardhi katika kipindi cha miaka miwili ya kwanza ya hatamu yetu katika Serikali.

'Hakuna maendeleo endelezi bila haki kamili katika Sera ya Kitaifa ya Ardhi'

Jina la Kiongozi wa Chama

Sahihi.....

Tarehe.....

Muhuri Rasmi wa Chama

Imeshudiwa na Mratibu wa Kitaifa wa KLA


Kwa niaba ya **Kenya Land Alliance (KLA)** na wanachama wake

Sahihi.....

Tarehe.....

Muhuri Rasmi

Mkataba huu ni chombo cha KLA kinachoshirikisha vyama vya kisiasa vitakavyojihusisha katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2007, kwa kuamini kwamba uhusiano na utekelezwaji wake na Viongozi wa Kisiasa utachangia kuwepo kwa uwajibikaji wa kisiasa katika mabadiliko ya ardhi yatakatayopelekea uzalishaji, usalama wa chakula, mapato bora, utumiaji endelezi wa ardhi na kukua kwa uchumi nchini Kenya.



**Kenya Land Alliance, C.K. Patel Building, 6th Floor, Kenyatta Avenue,
Nakuru. P. O Box 2177-20100 Nakuru, Kenya. Tel: 254-51-2210398
Telefax: 254-51-2215982 E-mail: klal@africaonline.co.ke or
info@kenyalandalliance.or.ke Website: www.kenyalandalliance.or.ke**